

SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P 327 GATUNDU

Kidato cha pili :tathmini la oktoba

Muda : saa 2

Jinadarasa:namb:.....

Binadamu ana kero, lindani na moyo wake,
Hupenda ya mororo, yote yasadifu kwake,
Yanoleta mataguro, hukwepa yasimfike,
Hiyo ni yake kasoro, kiumbe binadamu.

Milele katu hukiri, kupokonywa kilo chake,
Lakini huwa tayari, kudhulumu vya wenzake,
Na kujifanya hodari, kila lake liongoke,
Na hiyo yake kasoro, kiumbe binadamu.

Kutwaa asichopewa, pia ni tabia yake,
Ubishi kabarikiwa, hivyo ni vilima vyake,
Kama hayo kitendewa, hakiri ikubalike,
Pia ni kasoro yake, kiumbe binadamu.

Mwepesi wa kuchokoza, pia ni mtindo wake,
Ambaye hajamuanza, humtafutia lake,
Na puresha kamjaza, mradi akasirike,
Nayo ni kasoro yake, kiumbe binadamu.

Hakika binadamu, kwa ule uzito wake,
Kawekewa jahanamu, likawe ni pigo lake,
Hiyo siku ya hukumu, adhabu zikamfike,
Kwa zile kasoro zake, kiumbe binadamu.

Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (Alama 1)
.....
- b) Shairi hili ni la aina gani. Tolea sababu kwa jibu lako. (Alama 2)
.....
- c) Fafanua hulka/sifa ya binadamu kwa kutoa hoja tano. (Alama 5)
.....
.....
.....
.....
- d) Eleza umbo la shairi hili. (Alama 6)
.....
.....
.....
.....
.....
- e) Andika vifungu vifuatavyo kwa lugha sanifu. (Alama 4)
i) na puresha akamweka mradi akasirike.
.....
- ii) kupokonywa kilo chake.
.....

- f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na matumizi yake. (Alama 2)
- i) Mororo:.....
- ii) Mataguro:.....

MATUMIZI YA LUGHA

A.Akifisha: (Alama 3)

mimi sikuweza kutazama sinema litwayo star wars episode3 ingawa ilionyeshwa hapo mjini kwa miezi miwili ajaamong alitwambia

.....

.....

.....

B.Andika katika *udogo wingi*. (Alama 2)

Ngome ya mwanajeshi ilifanyiwa ukarabati.

.....

C.Bainisha ngeli za nomino hizi: (Alama 2)

- Chai.....
- Kiroboto.....
- Mtima.....
- Weledi:.....

D.Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao wa maneno. (Alama 2)

N + V + E + T + E + U + T + H + N + V

N + V + E + T + E + U + T + H + N + V

.....

E.Andika kinyume: (Alama 2)

Mwendapole alizama alipokuwa akichimba kisima cha Rafiki.

.....

F. Andika maneno *mawili* yaliyo na muundo wa silabi funge.

(alama.1)

.....

G. Onyesha muundo wa silabi ya *pili* katika maneno yafuatayo.

(Alama 1)

i) Mchwa :.....

ii)Kiota :.....

H.Bainisha mofimu *-LI-*katika tungo hili.

(Alama 3)

ALIVYOLIKIMBILIA

.....

I.Ainisha viwakilishi katika sentensi.

(Alama 2)

i) Wengi walihudumiwa na yeye.

.....

ii)Vyetu vilitengenezwa na huyu.

.....

J.Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni

(Alama 2)

Toa (tendeka):.....

Shona (tendesheana):.....

FASIHI

1)Fafanua sifa *tatu* za vitendawili,

(Alama 3)

.....

.....

.....

.....

2) Eleza dhima *mbili* za misimu katika jamii.

(Alama 2)

.....
.....

ISIMUJAMII

.....Keti chini haraka! Jina lako...wapi kitambulisho?...Hei afande ingiza hawa ndani...toa mshipi

Hii ni sajili gani?

(Alama 2)

.....

Eleza sifa zozote *tatu* za lugha ya aina hii.

(Alama 3)

.....
.....
.....

*****Heri njema*****